BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 19 Septemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 30 Juni, 2018.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

51. MHESHIMIWA KHADIJA OMAR KIBANO (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Tarehe 25/11/2017, maeneo mengi ya Unguja na Pemba ilinyesha mvua kubwa na baadhi ya maeneo kama Bububu na Kijichi mvua hizo zilisababisha mafuriko na vifo vya watu wawili, nyumba nyingi kuanguka pamoja na vitu vingi kuburutwa na maji na hadi hivi sasa tathmini ya maharibiko hayo inaonesha familia 90 ziliathiriwa na mafuriko hayo.

Je, ni muda gani malipo ya wahanga wa maafa hayo yatalipwa kwa walengwa hao.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

01 MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Siku za hivi karibuni Mji wa Zanzibar umekumbwa na matukio mengi ya uhalifu kama mauwaji, ubakaji, kupigwa watu, kuporwa n.k. Mafundisho ya dini ya Kiislamu yameeleza kuwa ulevi ni mama wa maasi, matukio hayo yanasababishwa na ongezeko kubwa la nyumba za ulevi (baa) ambazo zinachochea maasi ndani ya miji yetu hasa kwenye makaazi ya wananchi.

(a) Je, Serikali haioni muda umefika sasa wa kusitisha kabisa kutoa vibali vya kufunguliwa baa katika makazi ya watu.

(b) Je, hatua gani zinachukuliwa kudhibiti baa zilizopo ambazo vijana wengi wanakwenda kujifundisha kulewa na kushiriki matendo maovu kama vile uasharati, wizi, kukaba watu, fujo n.k

(c) Kwanini Serikali haiachani na mpango wa kutegemea mapato yanayotokana na baa na badala yake kubuni

vyanzo vyengine vya mapato kama vile kujengwa mikahawa ambayo watu watapata chakula n.k

50. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa zaidi ya miaka minane (8) iliyopita, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia mkataba na Serikali ya Misri kwa mashirikiano ya kuendeleza kilimo cha mboga mboga ambapo kwa upande wa Zanzibar kazi hiyo waliachiwa Jeshi la Kujenga Uchumi (J.K.U). Pamoja na nia nzuri ya Serikali zote mbili, mradi huo umekuwa na tija ndogo sana na kupelekea malalamiko juu ya umuhimu wa kuwepo mradi huo huko Bambi.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika na faida ya kiasi gani imepatikana kupitia mradi huo.

(b) Kwa kuwa mradi huo unasimamiwa na wataalamu kutoka Misri, Je, ni vijana wangapi wa Zanzibar wameweza kupata ujuzi kupitia mradi huo.

(c) Yapo madai ya udhalilishaji unayofanywa na wageni hao kwa vijana wetu, Je, Serikali inasemaje juu ya madai hayo.

Wizara ya Biashara na Viwanda

36. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Kwa kuwa kipindi cha Julai/Disemba, 2017 Wizara yako kupitia vyanzo vyake vya mapato ilijipangia kukusanya shilingi 236,201,769/-, lakini hadi kufikia Disemba, 2017 Wizara kupitia taasisi zake ilishakusanya jumla ya shilingi 621,897,246/- jambo ambalo ni zuri sana na la kupigiwa mfano kwa Wizara nyengine za Serikali.

(a) Je, vyanzo hivyo vya mapato ya Wizara vilifanya mkakati gani ulioweza kwa kipindi kifupi kukusanya mapato mara mbili ya makadirio yao.

(b) Je, kabla kulikuwa na tatizo gani ambalo lilisababisha kutofikia lengo la makusanyo wakati vyanzo vya mapato ni vile vile.

(c) Je, kuna motisha gani iliyotolewa kwa wafanyakazi wa Taasisi ambazo zimefanya vizuri ili kuongeza hamasa za ukusanyaji wa mapato ya Wizara.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

42 MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na mabadiliko ya Sera ya Elimu kwa wanafunzi ambao sasa wanatoka darasa la sita mpaka kidato cha kwanza baada ya kuondoshwa darasa la saba na darasa la sekondari maandalizi (orientation). Hata hivyo, mabadiliko hayo hayajazingatia kupunguzwa masomo mengi wanayosomeshwa wanafunzi wanapoanza skuli ya msingi na umuhimu wa somo la lugha ya kiingereza kuwa somo la lazima mwanafunzi kufaulu na kulijua kabla kwenda Sekondari.

(a) Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuwa wanafunzi watakapokuwa katika Skuli za Msingi wanasomeshwa masomo machache ya kuwatayarisha wavuke Sekondari wakiwa weledi na kuweza kukabili masomo ya Sekondari.

(b) Wizara imechukuwa mkakati gani kuhakikisha kuwa Wanafunzi wanaotoka darasa la sita kwenda Kidato cha kwanza, wamefaulu vyema na kujua masomo ya kiingereza na Hisabati ili waweze kukabiliana na mitihani ya kitaifa wakiwa Sekondari.

(c) Wizara imefanya tathmini yoyote kujua mfumo wa sasa wa kuwavusha wanafunzi wengi kutoka darasa la sita kwenda kidato cha kwanza wakiwa wana uwezo mdogo, unaathiri vipi matokeo ya mitihani ya kidato cha pili na cha nne.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

55 MHESHIMIWA KHADIJA OMAR KIBANO (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kuna sehemu mbali mbali za mji na vijiji ambazo zimekuwa na uchakavu wa mabomba unaotokana na miundombinu mibovu ya maji na kupelekea baadhi ya sehemu maji kuvuja ovyo na kutowafikia wananchi. Viongozi wa shehia wanaporipoti matatizo hayo, mamlaka husika (ZAWA) wanashindwa kufika maeneo husika.

Je, kwa nini Serikali kupitia Mamlaka ya Maji (ZAWA) hawawatumii mafundi bomba waliomo katika shehia kukabiliana na kadhia hiyo.

Wizara ya Afya:

40 MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali inastahili pongezi kwa kutoa huduma za afya bure. Pamoja na sera hiyo ya matibabu bure, hospitali za Serikali pia zinatoa huduma za afya kwa njia ya Bima ya Afya ambayo ni ya malipo. Aidha, kumekuwa na malalamiko kuwa huduma za afya kwa wenye Bima ya Afya katika hospitali za Serikali hazitolewi ipasavyo na kuwafanya wenye Bima ya Afya kukimbilia hospitali binafsi.

(a) Je, fedha hizo za Bima ya Afya zinaingia katika mfuko gani, wa Afya au wa Serikali.

(b) Je, kutoa huduma hiyo ya Bima ya Afya ina faida kwa Wizara au haina faida.

(c) Je, hatuoni kuwa kuifanya huduma ya Afya kuwa bure na upande mwengine kuwa na utaratibu wa Bima ya Afya ni kujichanganya.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

46. Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe Fuoni, wananchi wanaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuondoa tatizo la usafiri. Hata hivyo, bado kuna matatizo mengi ya ajali zinazosababishwa na madereva wazembe.

(a) Je, Wizara yako imejipanga vipi kuliondoa tatizo la ajali katika maeneo ya Meli Nne, Taveta, Kijitoupele, Mashine ya Maji na Kwandundu.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka matuta mapana ambayo hayataleta usumbufu kwa wasafiri wanaotumia barabara hiyo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

43. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vinavyoimarisha kilimo cha aina mbali mbali kama vile mboga mboga na kilimo cha miti ya matunda na viungo vya aina tofauti vinavyotumika katika mapishi ikiwemo hiliki, mdalasini na manjano.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi kulima hiliki, mdalasini na manjano.

(b) Je, Wizara inafahamu umuhimu wa zao la manjano katika mwili wa binaadamu.

(c) Na kama inafahamu, kwa nini kilimo hiki hakipewi kipaumbele.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
19 Septemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.